HALMASHAURI YA WILAYA MASASI

Simu: 023 - 2510031.
Fax: 023 - 2510031.
E-mail: ded@masasigo.tz
Website: www.masasidc.go.tz

S.L.P. 60,
Masasi,
Mtwara,
TANZANIA

# MAELEKEZO KUHUSU UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA WA MWAKA 2019 HALMASHAURI YA WILAYA YA MASASI

## A. UTANGULIZI

MSIMAMIZI WA UCHAGUZI HALMASHURI YA WILAYA YA MASASI KWA MAMLAKA ALIYOPEWA CHINI YA KANUNI YA TISA (9) YA KANUNI ZA UCHAGUZI WA MWENYEKITI WA KIJIJI, WAJUMBE WA HALMASHAURI YA KIJIJI NA WENYEVITI WA VITONGOJI ZA MWAKA 2019. ANAWATANGAZIA WANANCHI WOTE WA HALMASHAURI YA WILAYA YA MASASI KUJITOKEZA KWA WINGI KUGOMBEA NAFASI MBALIMBALI ZA UONGOZI PAMOJA NA KUCHAGUA VIONGOZI KWENYE UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA WA MWAKA 2019.

## B. YAFUATAYO NI MAELEKEZO YA UCHAGUZI KWA WANANCHI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA MASASI.

1. UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA WA MWAKA 2019 UTAFANYIKA SIKU YA JUMAPILI TAREHE 24/11/2019.
2. ZOEZI LA UANDIKISHAJI WAPIGA KURA LITAFANYIKA KWA MUDA WA SIKU SABA (7) KUANZIA TAREHE 08 OKTOBA, 2019 HADI TAREHE 14 OKTOBA 2019, VITUO VYOTE VYA UANDIKISHAJI VITAKUWA WAZI KUANZIA SAA MBILI KAMILI ASUBUHI NA KUFUNGWA SAA KUMI NA MBILI JIONI. VITUO VITAKUWA KWENYE MAJENGO YA UMMA AU SEHEMU ITAYOELEKEZWA NA MSIMAMIZI WA UCHAGUZI. IELEWEKE ZOEZI HILI LA UANDIKISHAJI WAPIGA KURA HALIHUSIANI NA ZOEZI LA UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA KWA MFUMO WA KIELEKRONIKI (BVR) LINALORATIBIWA NA TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI HAPA NCHINI KWANI BVR INATUMIKA KWENYE UCHAGUZI MKUU WA RAIS, WABUNGE NA MADIWANI NA SI UCHAGUZI HUU WA SERIKALI ZA MITAA WA MWAKA 2019.
3. UCHAGUZI UTAFANYIKA TAREHE 24 NOVEMBA, 2019. MAHALI ULIPOJIANDIKISHA NDIPO PATAKUWA KITUO CHAKO CHA KUPIGIA KURA HIVYO VITUO VYOTE VITAKUWA WAZI KUANZIA SAA MBILI KAMILI ASUBUHI HADI SAA KUMI KAMILI JIONI KWENYE MAJENGO YA UMMA AU ENEO ATAKALOELEKEZA MSIMAMIZI WA UCHAGUZI.
4. KILA MKAZI MWENYE SIFA ZIFUATAZO NDIYE ATAKAYESHIRIKI KUPIGA KURA

   A. AWE RAIA WA TANZANIA.

MSIMAMIZI WA UCHAGUZI
HALMASHAURI (W) MASASI

B. AWE MWENYE UMRI WA MIAKA WA MIAKA 18 AU ZAIDI.
C. AWE MKAZI WA KIJIJI AU KITONGOJI AMBACHO UCHAGUZI UNAFANYIKA.
D. ASIYE NA UGONJWA WA AKILI ULIOTHIBITISHWA NA DAKTARI ANAYETAMBULIKA NA SERIKALI AU BODI YA UTABIBU.
E. ASIWE AMEJIANDIKISHA KUPIGA KURA KATIKA KITUO ZAIDI YA KIMOJA.

5. MKAZI YOYOTE MWENYE SIFA ZIFUATAZO ANAYETAKA KUGOMBEA NAFASI YA UENYEKITI WA KIJIJI, UJUMBE WA HALMASHAURI YA KIJIJI, AU UENYEKITI WA KITONGOJI AJITOKEZE KUCHUKUA FOMU KWENYE OFISI YA MSIMAMIZI MSAIDIZI WA UCHAGUZI (OFISI YA KIJIJI) MAHALI WANAPOISHI. MKAZI YOYOTE ILI AGOMBEE ANAPASWA AWE;
   - RAIA WA TANZANIA
   - NA UMRI WA MIAKA 21 AU ZAIDI
   - ANAWEZA KUSOMA NA KUANDIKA KISWAHILI AU KIINGEREZA
   - NA SHUGHULI HALALI YA KUMWEZESHA KUISHI.
   - MWANACHAMA WA CHAMA CHA SIASA NA AMEDHAMINIWA NA CHAMA HICHO.
6. FOMU ZA KUGOMBEA UONGOZI/NAFASI YA MWENYEKITI WA KIJIJI, UJUMBE WA HALMASHAURI YA KIJIJI NA UENYEKITI WA KITONGOJI ZITACHUKULIWA NA KURUDISHWA KWENYE OFISI YA MSIMAMIZI MSAIDIZI WA UCHAGUZI (OFISI ZA VIJIJI) KUANZIA TAREHE 29 OKTOBA HADI TAREHE 04 NOVEMBA, 2019. AIDHA SAA KUMI KAMILI JIONI YA TAREHE 04 NOVEMBA, 2019 ITAKUWA TAREHE YA MWISHO YA KURUDISHA FOMU ZA KUGOMBEA.
7. FOMU ZOTE ZA KUGOMBEA ZILIZORUDISHWA KWA WAKATI ZITABANDIKWA KWENYE MBAO AU MAENEO YA MATANGAZO KWENYE OFISI YA MSIMAMIZI MSAIDIZI WA UCHAGUZI (OFISI ZA VIJIJI) AMBAPO SIKU YA UTEUZI WA WAGOMBEA WA UCHAGUZI ITAKUWA TAREHE 05 NOVEMBA, 2019.
8. MUDA WA KUWASILISHA PINGAMIZI DHIDI YA UTEUZI WA MGOMBEA YEYOTE UTAKUWA TAREHE 05 NOVEMBA HADI 06 NOVEMBA 2019.
9. KWA MGOMBEA AMBAYE HATARIDHIKA NA UAMUZI WA MSIMAMIZI MSAIDIZI WA UCHAGUZI KUHUSU UTEUZI ATAKUWA NA HAKI YA KUKATA RUFAA KWENYE KAMATI YA RUFANI KUANZIA TAREHE 05 NOVEMBA HADI TAREHE 08 NOVEMBA, 2019.MUDA WA KUSHUGHULIKIA RUFAA UTAKUWA NI KUANZIA TAREHE 05 NOVEMBA HADI TAREHE 09 NOVEMBA, 2019.
10. KAMPENI ZA UCHAGUZI ZITAFANYIKA KWA SIKU SABA KUANZIA TAREHE 17 NOVEMBA HADI TAREHE 23 NOVEMBA, 2019. MGOMBEA, WAWAKILISHI AU CHAMA CHA SIASA KINAWEZA KUITISHA MIKUTANO YA KAMPENI KWA KUFUATA RATIBA ITAKAYOWASILISHWA NA WAGOMBEA, WAWAKILISHI WAO AU VYAMA VYA SIASA NA KURATIBIWA NA MSIMAMIZI WA UCHAGUZI.

MSIMAMIZI WA UCHAGUZI
HALMASHAURI (W) MASASI

11. MPIGA KURA ILI AWEZE KUPIGA KURA ATAJITAMBULISHA KWA KUTUMIA KITAMBULISHO KIMOJAWAPO KATI YA VITAMBULISHO VIFUATAVYO;

A. KITAMBULISHO CHA MPIGA KURA
B. KITAMBULISHO CHA KAZI
C. HATI YA KUSAFIRIA
D. KADI YA BIMA YA AFYA
E. KITAMBULISHO CHA SHULE AU CHUO
F. KITAMBULISHO CHA MIFUKO YA HIFADHI YA JAMII
G. LESENI YA UDEREVA AU
H. KITAMBULISHO CHA TAIFA

NB: ENDAPO MPIGA KURA ATAKUWA HANA KITAMBULISHO CHA AINA YOYOTE LAKINI JINA LAKE LITAKUWEMO KWENYE ORODHA YA WAPIGA KURA, MSIMAMIZI WA KITUO ATAMRUHUSU KUPIGA KURA BAADA YA KUTAMBULIWA NA WAKAZI WA ENEO HUSIKA.

## C. LIFUATALO NI JEDWALI LA MTIRIRIKO WA MATUKIO YA UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA.

### JEDWALI LA MATUKIO

| Na | TUKIO | TAREHE | MHUSIKA |
|---|---|---|---|
| 1. | MAELEZO KUHUSU UCHAGUZI | 23 SEPTEMBA, 2019 | MSIMAMIZI WA UCHAGUZI |
| 2. | ZOEZI LA UANDIKISHAJI WAPIGA KURA | 8 – 14 OKTOBA, 2019 | MSIMAMIZI WA UCHAGUZI |
| 3. | KUBANDIKWA KWA ORODHA YA WAPIGA KURA | 15 OKTOBA, 2019 | MSIMAMIZI WA UCHAGUZI |
| 4. | UKAGUZI WA ORODHA YA WAPIGA KURA | 15 – 21 OKTOBA, 2019 | MSIMAMIZI WA UCHAGUZI |
| 5. | PINGAMIZI KUHUSU UANDIKISHAJI WA WAPIGA KURA | 15 – 21 OKTOBA, 2019 | MSIMAMIZI WA UCHAGUZI MSAIDIZI |
| 6. | UAMUZI KUHUSU PINGAMIZI | 21 – 22 OKTOBA, 2019 | MSIMAMIZI WA UCHAGUZI MSAIDIZI |
| 7. | MAREKEBISHO YA ORODHA YA WAPIGA KURA | 21 – 22 OKTOBA, 2019 | MSIMAMIZI WA UCHAGUZI MSAIDIZI |
| 8. | KUKATA RUFAA DHIDI YA UAMUZI WA PINGAMIZI | 21 – 23 OKTOBA, 2019 | MSIMAMIZI WA UCHAGUZI |
| 9. | UAMUZI WA RUFAA | 21 – 26 OKTOBA, 2019 | MSIMAMIZI WA UCHAGUZI |
| 10. | KUKOMA UONGOZI KWA VIONGOZI WALIOPO MADARAKANI | 22 OKTOBA, 2019 | MSIMAMIZI WA UCHAGUZI |
| 11. | KUCHUKUA FOMU ZA KUGOMBEA | 29 OKTOBA, 2019 | MSIMAMIZI MSAIDIZI WA UCHAGUZI |
| 12. | KUREJESHA FOMU ZA KUGOMBEA | 29 OKTOBA – 04 NOVEMBA, 2019 | MSIMAMIZI MSAIDIZI WA UCHAGUZI |



MSIMAMIZI WA UCHAGUZI
HALMASHAURI (W) MASASI

| | | | |
|---|---|---|---|
| 13. | UTEUZI WA WAGOMBEA | 5 NOVEMBA, 2019 | MSIMAMIZI MSAIDIZI WA UCHAGUZI |
| 14. | UWASILISHAJI WA PINGAMIZI KUHUSU UTEUZI | 5 – 6 NOVEMBA, 2019 | MWOMBAJI/MGOMBE A |
| 15. | UAMUZI WA PINGAMIZI KUHUSU UTEUZI | 5 – 7 NOVEMBA, 2019 | MSIMAMIZI WA UCHAGUZI MSAIDIZI |
| 16. | KUKATA RUFAA DHIDI YA UAMUZI KUHUSU PINGAMIZI LA UTEUZI | 5 – 8 NOVEMBA, 2019 | MWOMBAJI/MGOMBE A/MSIMAMIZI WA UCHAGUZI |
| 17. | UAMUZI WA KAMATI YA RUFAA | 5 – 9 NOVEMBA, 2019 | KAMATI YA RUFANI |
| 18. | UWASILISHAJI WA RATIBA ZA MIKUTANO YA KAMPENI KUTOKA KATIKA VYAMA VYA SIASA | 10 NOVEMBA, 2019 | VYAMA VYA SIASI/MSIMAMIZI WA UCHAGUZI |
| 19. | UWASILISHAJI WA RATIBA ZA MIKUTANO YA KAMPENI KWA MKUU WA POLISI WA WILAYA | 14 NOVEMBA, 2019 | MSIMAMIZI WA UCHAGUZI |
| 19. | KUANZA KWA KAMPENI | 17 – 23 NOVEMBA, 2019 | MSIMAMIZI WA UCHAGUZI |
| 20 | SIKU YA UCHAGUZI | 24 NOVEMBA, 2019 | MSIMAMIZI WA UCHAGUZI |

**KAULI MBIU YA UCHAGUZI HUU WA SERIKALI ZA MITAA WA MWAKA 2019 "VIONGOZI BORA WA SERIKALI ZA MITAA NI CHACHU YA MAENDELEO NI HAKI NA WAJIBU KUJIANDIKISHA, KUGOMBEA NA KUCHAGUA KIONGOZI BORA".**

**MAELEKEZO HAYA YAMETOLEWA LEO TAREHE 23/09/2019 NA.**

**JEREMIAH J. LUBELEJE**
**MSIMAMIZI WA UCHAGUZI (H/W)**
**MASASI**

MSIMAMIZI WA UCHAGUZI
HALMASHAURI (W) MASASI